

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TANGAZO LA KUITWA KAZINI**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa pamoja kwa kupitia mradi wa Mfuko wa Dunia wa kupambana na magonjwa ya Kifua Kikuu, Malaria na HIV/AIDS (GFATM) na Mradi wa Mkapa Fellows Program Awamu ya Tatu, inapenda kuwataarifu waombaji waliomba nafasi mbalimbali za kazi kuanzia tarehe **22 Julai, 2019** hadi tarehe **05 Agosti, 2019** kupitia OR - TAMISEMI kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika hivyo wanatakiwa kuripoti kazini.

Waombaji wote waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

- i) Kufika **Chuo cha Mipango Dodoma** tarehe **28/10/2019** ili kukamilisha taratibu za ajira zao za mikataba pamoja na kufanyiwa mafunzo elekezi. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi kwa tarehe hiyo bila ya taarifa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Kuwasilisha vyeti halisi (**Originals Certificates**) vya masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea kwa ajili ya kuhakikiwa kabla ya kupewa barua za ajira.
- iii) Kuwasilisha cheti cha usajili/leseni, cheti cha mazoezi kwa vitendo (internship) kwa kada zinazohusika kama vile madaktari, wafamasia, wateknolojia na wauguzi.
- iv) Picha mbili (2) ya ukubwa wa Pasipoti na maelezo binafsi (CV yakionesho umri, anuani kamili ya Posta, barua pepe na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/ namba ya kiganjani ya wadhamini wasiopungua watatu (3).

- v) Hakutakuwa na mabadiliko ya vituo, hivyo watakaoshindwa kuripoti katika muda uliopangwa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.

Orodha ya majina ya watumishi wote waliopangiwa vituo vyatuzi yanapatikama kupitia tovuti ya OR - TAMISEMI: [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz). na Benjamin Mkapa Foundation: [www.mkapafoundation.or.tz](http://www.mkapafoundation.or.tz).

Aidha, tunapenda kuwafahamisha wote waliopangiwa kazi kuwa, ajira hizi ni za mkataba na zinasimamiwa na Taasisi ya Benjamin Mkapa kupitia mradi wa Global Fund na Mradi wa Mkapa Fellows Awamu ya Tatu. Vilevile, tunapenda kuwafahamisha kuwa pamoja na kwamba ajira hizi ni za mkataba, kabla au baada ya kukamilika kipindi cha mkataba, waajiriwa wote katika miradi tajwa **wanaweza kupata nafasi ya kujiunga** katika Utumishi wa Umma kulingana na taratibu za ajira za Serikali iwapo kibali cha ajira kitatolewa.

Waombaji wote waliochaguliwa wanombwa kutoa taarifa ya kukubali kwao ndani ya siku saba kupitia anuani ya barua pepe ifuatayo: [info@mkapafoundation.or.tz](mailto:info@mkapafoundation.or.tz) na kisha kufika **Chuo cha Mipango Dodoma tarehe 28 Oktoba, 2019 saa 2:30** asubuhi kwa ajili ya taratibu nyingine za ajira.

#### **Limetolewa na:-**

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamin Mkapa

**22/10/2018**

